

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA HABARI UTAMADUNI SANA NA MICHEZO**

Simu: 2126826

Fax: 2126834

E-Mail: km@habari.go.tz

Tovuti: www.habari.go.tz



Jengo la LAPF

Ghorofa ya 8

Mtaa wa Uhindini Makole

S. L. P. 25,

DODOMA

26 Septemba, 2017.

TAARIFA KWA UMMA.

**WADAU KUKUTANA KUJADILI KANUNI ZA MAUDHUI YA UTANGAZAJI NA
MITANDAO YA KIJAMII.**

Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo imeandaa kikao cha Wadau cha kupitia Rasimu za maudhui ya utangazaji (Broadcasting Services Content Regulations) na mitandao ya kijamii (Online Content Regulations), 2017.

Kikao hicho Kitafanyika tarehe 28 Septemba, 2017 katika ukumbi wa Mwalimu Nyerere Convention Centre (JKNCC), Jijini Dar - es- Salaam kuanzia saa 4:00 asubuhi kikiwashirikisha Wamiliki na Watendaji Wakuu wa Redio, Televisheni, Mitandao ya Kijamii na wadau wengine wa sekta ya Habari.

Lengo la kikao hicho ni kupata maoni ya wadau kuhusu rasimu hizo za Kanuni mpya. Kama mdau wa Utangazaji unaombwa kushiriki kwa kutoa maoni (Oral submission) au kwa njia ya maandishi (written submission).

Rasimu hizo zinapatikana katika tovuti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kubofya www.habari.go.tz kisha ingia sehemu ya machapisho bofya kipengele cha Sera, Kanuni na Sheria , na www.tcra.go.tz.

Kikao hicho kitafunguliwa na Katibu Mkuu Wizara ya Habari Utamaduni Sanaa na Michezo Prof. Elisante Ole Gabriel.

Wadau wote wanakaribishwa kushiriki katika mkutano huo muhimu.

Imetolewa na :

Lorietha Laurence

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano Serikalini

Wizara ya Habari Utamaduni Sanaa na Michezo.